# MAGAZETINI WIKI HII

Mji wa Serikali, Mtumba S.L.P. 315, DODOMA. Simu: +255 26 2310021 Barua pepe: km@sheria.go.tz




Constitution and Legal Affairs ministry permanent secretary Mary Makondo (L) chairs the 7th Emergency Session of the African Union's Professional Committee of Government Legal Experts on Justice and Law which opened in the Ghanaian capital, Accra, on Monday. Photo: Correspondent Lusajo Mwakabuku

The Guardian Pg. 2 18 January, 2023

## MAHAKAMA



JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, akisalimiana na maofisa wa mahakama hiyo, alipowasili katika Kituo Jumuishi Temeke, Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, kuzungumza na waandishi wa habari kuhusu Siku na Wiki ya Sheria nchini inayotarajia kuanza Januari 22, mwaka huu. (Picha na Rehema Mohammed).




Vaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama (kakati) akikata utepe wakati wa uzinduzi wa Mfuko wa Faida (Faida Fund), uliofanyika kwenye ukumbi wa imataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam, Januari 14, 2023. Pamoja naye ni Vaziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro (watano kushoto), Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti a Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deo Ndejembi (wanne kushoto), Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Natu El-Maamry Mwamba (watano kulia) pamoja na viongozi wengine. **PICHA: MPIGA PICHA VETU**

Nipashe Januari 18 Uk. 9

# Spika aweka msimamo sheria za kupambana na ukatili kijinsia

**Na Hamida Kamchalla,**
TANGA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema Bunge liko tayari kurekebisha au kufuta kabisa baadhi ya vipengele vya sharia vinavyowapa faida kisheria wanaofanya makosa ya ukatili wa kijinsia nchini kukwepa adhabu.

Aidha, amesema Bunge litafanya hivyo wakati wowote kuanzia sasa kama serikali itaamua kupeleka Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ili kufumuliwa na kutungwa mpya zinazodhibiti vitendo hivyo.

Dk. Tulia alikuwa akizungumza jana jijini Tanga hapa alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa 11 wa Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA).

"Kutokana na udhaifu wa kisheria unaoonekana katika baadhi ya sheria. Nawasihi TAWJA kuainisha vipengele mnavyoona vinamlinda mtuhumiwa kwa kutoa mwanya wa kuachiwa huru, wakati kosa limefanyika.

"Iombeni serikali ilete marekebisho ya vipengele hivyo bungeni ili viangaliwe na kutungwa upya ili haki ipatikane kwa pande zote. Tumalize haya malalamiko ya wananchi kwa kuwaondolea maswali yasiyojibika," alisema.

Dk. Tulia alisema kwa kawaida wananchi wanapomkamata mhalifu aliyefanya ukatili, humpeleka polisi wakijua atafunguliwa mashtaka na kufikishwa mahakamani na kisha kupewa adhabu. Lakini cha ajabu baadaye hushangaa ameachiwa huru, hivyo kuibua maswali na masononeko kwa walliomkamata.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, akizungumza katika mkutano huo, alisema TAWJA imeanza kufanyia kazi kwa vitendo maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa mwanzoni mwa mwaka huu.

Prof. Juma alisema TAWJA pamoja na mahakama, kazi kubwa wanayofanya ni utoaji haki na kuelimisha umma kuhusu utoaji wa haki za binadamu, kujenga uwezeshaji miongoni mwa wadau wa haki za binadamu, upatikanaji wa haki kwa makundi yaliyoko katika hali hatarishi, wanawake,. watoto na watu wenye ulemavu.

"Sisi mahakama tunajivunia sana uwepo wa hiki Chama cha TAWJA, muhimili wa mahakama unakichukulia kama chombo maalumu ambacho kinaleta taswira na muonekano kwamba, mahakama ni taasisi inayojali usawa wa kijinsia na kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa TAWJA, Jaji Joaquine De- Mello, alisema chama hicho kilianzishwa mwaka 200 kama chama cha kijamii, dhima yake kuu ni kusimamia haki na kuona haki sawa zinatolewa kwa wote, kwa kuzingatia utawala wa sheria na usawa wa kijinsia.

# Jaji Kiongozi kuzindua majengo ya mahakama

**NA MWANDISHI WETU**, *Katavi*

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mustapher Siyani, anatarajiwa kesho kuzindua majengo matatu ya Mahakama za Hakimu Mkazi.

Uzinduzi huo utafanyika katika viwanja vya jengo jipya la Mahakama ya Hakimu Mkazi Katavi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mahakama ya Tanzania, majengo mapya matatu yatakayozinduliwa ni Mahakama ya Hakimu Mkazi Katavi, Lindi na Songwe.

Ilisema majengo hayo yamejengwa kwa kutumia fedha za ndani na ni mwendelezo wa uzinduzi wa miradi ya majengo ya mahakama yanayozinduliwa maeneo mbalimbali nchini.

Taarifa hiyo ilisema kukamilika kwa ujenzi wa miradi hiyo umezingatia mahitaji ya kisasa kwa wadau wa mnyororo wa utoaji haki.

Ilisema katika majengo hayo kuna ofisi za mawakili, maofisa Magereza, ustawi wa jamii, maeneo kwa watu wenye mahitaji maalumu na watoto wamewekewa vyumba vya kutumia wakiwa mahakamani.

Iliongeza kuzinduliwa kwa majengo hayo katika mikoa hiyo mitatu kutaongeza ufanisi na utoaji huduma kwa wananchi kwa kuwa yana mazingira rafiki ya utoaji wa huduma kwa kutumia mfumo ya kiteknolojia ya habari na mawasiliano.

Halfa ya uzinduzi inatarajiwa kuhudhuriwa na viongozi waandamizi mbalimbali wa mahakama, serikali na Bunge.

# Samia appoints chairpersons of two bodies

**By DAILY NEWS Reporter**

PRESIDENT Samia Suluhu Hassan has made appointments of Chairpersons of two institutions and extended the tenure of Chairperson and Vice-Chairperson of the Commission for Human Rights and Good Governance (CHRAGG) for a second term.

Nipashe Januari 18 Uk. 9

A statement issued by the Directorate of Presidential Communications on Monday said Dr Samia has as well appointed four commissioners of CHRAGG.

According to the statement, President Samia has appointed Prof Ahmed Mohamed Ame to become Board Chairman of Land Transport Regulatory Authority (LATRA).

Prof Ame currently works as a lecturer at the University of Dar es Salaam and takes over the position from Eng John Ndunguru.

Dr Samia has also appointed former Director General of Public Service Social Security Fund (PSSSF), Mr Eliud Sanga, to become Board Chairman of mobile phone operator, Airtel Tanzania. Mr Sanga replaces Gabriel Malata, who was last year appointed a judge of the High Court.

In a related development, President Samia has extended the tenure of Judge (rtd) Mathew Mwaimu and Mr Mohamed Khamis Hamadi, to serve as Chairperson and Vice-Chairperson of CHRAGG for a second term, respectively.

The statement noted further that Dr Samia has also appointed four commissioners for human rights and good governance for CHRAGG effective from January 15, this year.

The commissioners include Mr Thomas Masanja, Ms Amina Talib Ali, Mr Khatibu Mwinyi Khatibu and Mr Nyanda Shughuli.

CHRAGG is an independent government department, established as the national focal point for the promotion and protection of human rights in Tanzania.

The commission covers a wide range of functions with the core functions of promoting and protecting human rights.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

# TAARIFA KWA UMMA

Mahakama ya Tanzania inawatangazia Wananchi wote kuwa Wiki ya Sheria itaadhimishwa nchini kote kuanzia tarehe 22 Januari, 2023 hadi tarehe 29 Januari, 2023.

Wiki hii itaadhimishwa Kitaifa jijini Dodoma katika Viwanja vya Nyerere 'Square' ambapo kutakuwa na Maonesho ya Shughuli mbalimbali za kimahakama. Wiki ya Sheria inatarajiwa kuzinduliwa kwa Matembezi Maalum yatakayofanyika Siku ya Jumapili tarehe 22 Januari, 2023 Saa 12:00 asubuhi. Matembezi hayo yataanzia Viwanja vya Kituo Jumuishi Cha Utoaji Haki (IJC) Dodoma na kuishia Viwanja vya 'Nyerere Square'. Matembezi hayo yataongozwa na Mhe.Dkt. Phillip Isdori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wadau watakaoshiriki kwenye Maonesho ni Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Chuo Cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mamlaka ya Usimamizi Bandari Tanzania na wengine.

Ndugu Mwananchi, endapo una shida yoyote ya Mambo ya Kisheria, maoni au mapendekezo ya Uboreshaji wa Huduma za Mahakama tafadhali fika kwenye Viwanja vya Maonesho ili upate ushauri na huduma mbalimbali za Kisheria kutoka kwa Majaji, Wasajili, Mahakimu, Watendaji na Wadau wengine wa Mahakama watakaokuwa kwenye Viwanja vya Maonesho.

Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yatahitimishwa na Kilele cha Siku ya Sheria nchini tarehe 01 Februari, 2023, kuanzia saa 03:00 Asubuhi katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma. Mgeni rasmi katika Maadhimisho hayo ni Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kauli mbiu ya Wiki na Siku ya Sheria 2023 ni; 'Umuhimu wa utatuzi wa Migogoro kwa njia ya Usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu: Wajibu wa Mahakama na Wadau.'

**Wote mnakaribishwa.**

**Imetolewa na;**